# Jinsi ya Kutengeneza Kilishio chako cha nyuki

## Kujenga kilishio

Hakikisha kuwa una kila rasilimali na uwe na ujuzi kuhusu vipimo vya kilishio utakachotengeneza. Kata sanduku katika vipimo sahihi na laini pande zote za mbao zilizokatwa. Tengeneza kingo nzuri kando ya vipande vya mbao vilizyokatwa ili kusahihisha vipimo vyako. Panga mbao zilizokatwa na kulainishwa na uziweke juu ya kisanduku na upime vipimo vya ndani kwani unene wa ubao hutofautiana kila wakati. Wakati mbao zote zimekatwa na kupangwa, zigandishe na kuzibana na uzifunge  kwa kutumia misumari ili kuzishikanisha pamoja. Pia, ongeza silikoni ili kuziba mashimo nyuso zote za ndani ili kuzuia mende na panya.

## Kuweka kilishio juu ya mzinga

Unganisha kiyeyusho chako, na nyenzo zote zinazohitajika na kisha weka kilishio juu ya mzinga. Kumbuka kuweka baadhi ya viunzi au fremu zilizopakwa nta kwenye mzinga. Weka mchanganyiko wa kipimo kimoja cha sukari na kipimo kimoja cha maji kwenye kilishio ili hata mvua inaponyesha, nyuki wapate maji ya sukari. Unaweza pia kuweka mikate ya protini chini kilishio ili wakati nyuki hawali protini, huwa wanaweza kupata sharubati ya sukari.